MSEA
MICRO AND SMALL ENTERPRISES AUTHORITY

# MKATABA WA HUDUMA

## UJUMBE WETU

Biashara za Rejareja na Ndogondogo zenye Hadhi ya Kimataifa

## MALENGO YETU

Kuimarisha ukuaji wa Biashara za hadhi na endelevu za Rejareja na Ndogondogo

## THAMANI KUU

- Uzingatiaji Mteja
- Umbuji na Ubunifu
- Uwajibikaji na Maadili
- Utaalamu
- Ushirikiano na Ujumuishaji

## JUKUMU LETU

Kushirikisha, kuwianisha na kuwezesha uoanishaji wa shughuli mbalimbali, miradi na mipango ya ustawi ya sekta za umma na binafsi inayohusiana na Biashara Rejareja na Ndogondogo.

| | AINA YA HUDUMA INAYOTOLEWA | VINAVYOHITAJIKA | ADA (IWAPO IPO YOYOTE) | KIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kusajili Mashirika Makuu ya MSE | • Fomu ya maombi iliyojazwa ipasavyo (FORM A)<br>• Fomu iliyojazwa ipasavyo baada ya kufahamu iliko ofisi iliyosajiliwa pamoja na anwani ya posta (FORM B)<br>• Nakala ya katiba,<br>• Orodha ya viongozi wa mpito | Ksh. 2000.00 | Katika muda wa siku 60 |
| 2 | Kusajili Vyama vya MSE | • Fomu ya maombi iliyojazwa (Form A)<br>• Nakala ya katiba,<br>• Orodha ya viongozi wa mpito | Ksh. 2000 | Katika muda wa siku 60 |
| 3 | Kujaza fomu za ushuru kutoka kwa Mashirika Makuu ya MSE | • Vitabu vya Uhasibu Viliyokaguliwa<br>• Orodha ya wanachama<br>• Orodha ya washikilizi wa ofisi<br>• Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Mwaka (AGM) | • Ksh. 1000 kwa wanachama wasiozidi 35.<br>• Ksh 2000 kwa wanachama 36 hadi 1000<br>• Ksh 3000 kwa wanachama wanaozidi 2000 | Siku 7 |
| 4. | Kujaza fomu za ushuru kutoka kwa Vyama vya MSE | • Vitabu vya Uhasibu Vilivyokaguliwa<br>• Orodha ya wanachama<br>• Orodha ya viongozi walio ofisini<br>• Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Mwaka | • Ksh. 1000 kwa wanachama wasiozidi 35.<br>• Ksh 2000 kwa wanachama 36 hadi 1000<br>• Ksh 3000 kwa wanachama wanaozidi 2000 | Siku 7 |
| 5 | Kuwapa mafunzo ya Usimamizi viongozi wa Vyama vya MSE | Maombi rasmi kutoka kwa chama cha MSE kilichosajiliwa | • Ksh 300 kwa kila kiongozi kwa ajili ya mafunzo ya siku 3. | Siku 7 |
| 6. | Kuwapa mafunzo ya Usimamizi viongozi wa SACCO za MSE | Maombi rasmi kutoka kwa SACCO ya MSE iliyosajiliwa | • Ksh 300 kwa kila kiongozi kwa ajili ya mafunzo ya siku 3 | Siku 7 |
| 7 | Kuwapa mafunzo ya ujasiriamali | Maombi rasmi kutoka kwa MSE mbalimbali (MSEs) au Chama cha MSE | Bila malipo | Saa 24 |
| 8 | Kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu, ushauri nasaha na uleaji vipaji | Maombi rasmi kutoka kwa MSEs na Chama cha MSE | Bila malipo | Saa 24 |
| 9 | Kushirikisha MSEs pamoja kwa lengo la kuzipa usaidizi wa kiufundi/kitaalamu kuhusu ustawishaji wa bidhaa | Maombi rasmi kutoka kwa MSEs au Chama cha MSE | Bila malipo | Siku 14 |
| 10 | Kutoa huduma za ulezi wa biashara changa | Maombi rasmi kutoka kwa MSEs | • Ksh5000 kwa Mwezi kwa mpango wa mwaka 1 (eneo lililo wazi)<br>• KSh10,000 na zaidi kwa mwezi kwa mpango wa mwaka 1 (katika hafla za maonyesho) | Siku 15 |
| 11 | Kuwezesha uboreshaji wa ujuzi wa kiufundi | Maombi rasmi kutoka kwa MSEs | • Ksh500 ambayo ni ada ya kutuma maombi<br>• Ksh 3000 kwa mwezi kwa ajili ya mafunzo ya miezi 3 | Punde tunapopata darasa la washiriki wasiopungua 15 |
| 12 | Kuwezesha uenezaji wa teknolojia | Barua rasmi ya warejelewa kutoka kwa chama/shirika la kimsingi, taasisi, shirika au afisa wa ustawishaji biashara wa kaunti | • Ksh50 kwa kila saa kwa muda usiozidi jumla ya saa 20 kwa wiki | Punde tunapofikisha darasa la washiriki wasiopungua 5 |
| 13 | Kutoa vifaa vya matumizi maalum kwa MSE za Kituo cha Ufanisi (COE) cha Kariobangi MSE | Kadi ya kazini iliyojazwa maelezo ipasavyo | **Mashine**<br>• Mashine za kukata vyuma@ Ksh250 kwa saa<br>• Mashine za kuchonga mbao, vyuma n.k @ Ksh250 kwa saa<br>**Uchomeleaji kwa moto wa Arc**<br>• Kati ya 1.4mm hadi 4mm@Ksh 4 kwa kila inchi<br>• 4mm hadi 6mm @Ksh6 kwa kila inchi<br>• 6mm hadi 10mm @Ksh10 kwa kila inchi<br>• 10mm na zaidi @Ksh20 kwa kila inchi<br>**Vifaa**<br>• Jeki @Ksh500 kwa siku<br>• Mashine ya Kuchomelea @ Ksh.500 kwa siku<br>• Grainda ya mkononi @ Ksh500 kwa siku<br>• Mtungi wa kuhifadhi hewa/gesi almaarufu Air Compressor @ Ksh500 kwa siku<br>**Kazi za Kujenga Mwili wa Gari**<br>• **Basi dogo** (Minibus)- La Abiria 28 @ Ksh20,000<br>• **Basidogo**- Abiria 40 @ Ksh26,000<br>• **Lori** tani 3 Ksh12,000<br>• **Lori** tani 7 Ksh18,000 | Inaendelea |
| 14 | Kuandaa hafla za maonyesho na maonyesho ya biashara ili kufikia masoko ya ndani ya nchi | Maombi rasmi kutoka kwa MSEs<br>Bidhaa za Ubora wa juu kutoka kwa MSEs | Ksh1000 | Mara moja kwa mwaka katika kila kaunti |
| 15 | Kuandaa hafla za maonyesho na maonyesho ya biashara ili kufikia masoko ya ukanda | Maombi rasmi kutoka kwa MSE mbalimbali<br>Bidhaa zenye Ubora wa juu kutoka kwa MSEs | Ksh2500 | Mara moja kwa mwaka |
| 16 | Kutambua masoko palipo na uwezekano wa kununua bidhaa za MSE | Maombi rasmi ya MSE<br>Bidhaa za Ubora wa juu kutoka kwa MSEs | Bure | Inaendelea |
| 17 | Kuzitengea MSEs maeneo mwafaka na ya bei nafuu ya kufanyia kazi | • Uwepo wa ardhi ya kujenga/kustawisha maeneo ya kikazi ya MSE.<br>• Shughuli za MSE katika maeneo jirani | • Kodi zifaazo zilizowekwa na kamati simamizi za maeneo hayo | Inaendelea |

*Ujasiriamali Unaokuza Kenya*

P. O. Box 48823-00100, Nairobi, Gen Line: +254 20 3340 006 / 0700 666 000
Email: info@msea.go.ke Website: www.msea.go.ke